# *Jiwe la kiroho la kujengea na. 140*

*KUINGIA KATIKA USHIRIKA HALISI*

"*Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli; bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo mwana wake, yatusafisha dhambi zote" (1Yohana1:3-7)*

Hili ndilo alilosema Nabii wa Mungu juu ya hilo. Ni sawa na hawa wanandoa wadogo ambao nilikuwa ninawazungumzia walipoowana hilo sio jambo lote hawajafanya chochote ila wamefanya tu sherehe. Mhudumu amesema tu, "Ninawatangaza ninyi kama mume na mke"bado haijawa tayari. Anafanya nini? Anamchukua kwenye nyumba yake aliyoiandaa kwa ajili ya mkewe.

Sasa, watu wengi hapa wanaweza wasikubaliane na mimi kwa hili, lakini huishi ila kwenye nyumba ya vyumba

vitatu unaweza ukawa na vyumba vingi. Lakini hasa unavyo vyumba vitatu tu. Hivyo ni Jiko, chumba cha kupumzikia na chumba cha kulala .Unaweza ukawa na vyumba vitatu au vinne na unaweza ukawa na jiko na chumba cha kulia chakula nakadhalika, lakini kwa uhakika mtu anaishi katika nyumba ya vyumba vitatu. Unaishi kwenye nyumba ya vyumba vitatu katika mwili wako; nafsi, mwili na roho. Mungu anaishi katika nyumba ya vyumba vitatu Baba, mwana, na Roho Mtakatifu kila kitu katika tatu.

Sasa, mwanamke anapochukuliwa, Bibi arusi mdogo (oh, jinsi bwana arusi anavyompenda bibi arusi), lakini bado, hawako kwenye ushirika mkamilifu wa kweli. Sasa jambo la kwanza…..Jikoni tunafanya nini? Ndipo ambapo tunalia chakula. Hivyo ndivyo ilivyo katika chumba cha kwanza cha kanisa. Unakula hapa unakuja unakaa kiti cha nyuma, unasikiliza neno, na jambo la kwanza unajua unaanza “Oh Mungu, hiyo ilimaanisha mimi” Unampokea Yeye kama mwokozi wako binafsi; kwa imani umelishikilia hilo. Hapo sasa unaanza kula

Neno unaanza kujisikia kwamba umempokea Kristo kama mwokozi wako. Unaanza karamu katika Neno; unalifurahia hilo..Ulizoea mhubiri akizungumza Neno hukulifurahia unainuka na kutoka nje ya jengo …siyo sahihi. Unainuka na kutoka nje Lakini baada ya kumpokea Kristo, hapo umetengwa sasa. Maji ya Neno ya farakano yamekutenga na kuwaza kwako maovu (Waefeso 5:25 - 27).

Sasa kitu kinachofuatia ni mahali pa kupumzikia (sebuleni) ambapo unamchukua bibi arusi wako mdogo, Anaondoa kitambaa chake kinachomfunika unakuja karibu kidogo. Unapofanya hivyo unaweka mkono wako kumzunguka yeye unazungumza naye, unamkumbatia…..Hayo ndiyo yanayokuja katika ushirika na Bwana Yesu kabla hujafanya hivyo unatengwa kutoka kwenye dhambi zako halafu unakumbatia injili ya Bwana. Unakumbatia Neno lililoandikwa unaliamini hilo kwa moyo wako wote.”Mungu haijalishi unataka mimi nifanye nini, chochote ulichonipangia maishani niko tayari sasa kukipokea hicho ”hapo ni

mahali pakupumzika (sebuleni) halafu bado unasema je hapa siyo mbali nyakutosha?" hapana Bwana.

Chumba kinachofuatia ni chumba cha kulala sasa unapoingia katika chumba cha kulala, hapa unakuja kwenye ushirika na uhusiano. Unakuwa kwenye uhusiano, Sasa mnao ushirika mkamilifu kwa sababu hamwezi kuwa na ushirika mkamilifu mpaka muwe na uhusiano. Kila mtu ajua hilo.

Na sikiliza hivyo ndivyo ilivyo na kanisa leo tunao watu wengi tunao watu wengi ambao wanaona aibu kuingia kwenye ushirika mkamilifu na Mungu kwenye maisha mapya na kuzaliwa mara ya pili kama tu Bibi Arusi wa Kristo sasa kwa nini hatuingii kwenye uhusiano, aibu zote na kurudi nyuma kote na vyote viondoke kutoka kwetu? Kama tunakuja kwenye ushirika mkamilifu tunazaliwa mara ya pili sijalishi … Raisi wa America (U.S.A) anaweza akawa amesimama barabarani utampigia Mungu kelele."Haleluya, Bwana asifiwe halleluya" Hujali kwa sababu umekuja kwenye ushirika umezaliwa mara ya pili wewe ni mtoto mpya uko kwenye

utukufu wa shekinah pamoja na Mungu mkishirikiana pamoja naye. Tunachohitaji leo. Ndugu ni ibada chini ya damu ibada katika uhusiano mkamilifu kufa kabisa.

Mungu amewaweka watoto wake hapa, sifa zake, ili wawe na ushirika naye kwa kusikia Neno lake.

Nilikuwa ninazungumza na mwinjilist maarufu, ndugu yangu T. L. Osborn. "Alisema, nilikuwa ninafikiria, ndugu Branham, vile ambavyo lengo langu lote ni kuokoa nafsi na kutoa muda wangu wote kuokoa nafsi kwa Kristo" nikasema,"Nikafikiria, vipi upendo wangu na kujitoa kwangu kwa Kristo? "Kristo anampenda yeye pia. Anatupenda sisi Tunaweka muda mwingi na mambo, lakini Mungu anatutaka tukae pekee, na kuketi chini na kumwabudu yeye, na kuzungumza naye kuyazungumza yote. Nalipenda hilo oh, huo uzuri. Huo ni wakati mkuu sana katika maisha ya mtu yoyote ni kukaa chini na kutafakari, ondoa kila kitu katika mawazo yako (Zaburi 73:28).

Kama mwanaume au mwanamke amewahi kuwa na ushirika hasa akaonja ushirika wa kiungu na Kristo, ni afadhali niwe na huo kulikoni likizo zote na mambo ya dunia. (Wafilipi 2:1-3) hakika kama unataka kunipa kitu cha kunipumzisha, hebu nipate mguso wa Kristo. Hebu niache nizungumze naye kidogo na mizigo yangu iondolewe. Imekwisha. Hapana ….ni afadhali nizungumze naye kuliko kitu kingine nijuacho duniani, niwe na ushirika pamoja naye.

Yesu aliomba kitu kimoja tu katika maombi yake kwa baba unajua ilikuwa ni nini? Kitu kimoja baada ya sadaka yake yote aliyoifanya hapa duniani, maisha alivyoishi, njia aliyoipitia, aliomba kitu kimoja "kwamba nilipo mimi nao watakuwepo pia" yeye aliomba ushirika wetu hilo ni jambo pekee alilomuomba baba katika maombi yake uwe mshirika wake milele. Kama unataka kusoma hilo ni Mt. Yohana 17 na mstari wa 24….. sasa tunapaswa kumhitaji yeye kwa kiasi gani?

Sasa, sikiliza, kama umezaliwa kweli na Roho wa Mungu, hilo linamaanisha kila kitu kwako

siyo kitabu cha sheria, kuamini kwako. Huishi kwa sheria zozote na kadhalika; unaishi kwa neema ya Mungu, Roho wa Mungu.

Kama kuna baadhi hapa, Bwana, ambao hawajaingia katika ushirika huu mkuu ndani ya Kristo, tunaomba kwamba usiku wa leo watafanya uamuzi ule wa milele, wajazwe na Roho wa Mungu.

Ndugu Braham alisema; hapa ni mahali palipo wazi/huru (maskani) Haijawa dhehebu kamwe, na Mungu ajalie lisije likawa. Kwa sababu tunataka mahali hapa pawe ni mahali ambapo hatuna sheria, ila upendo, hakuna kanuni bali Kristo, hakuna kitabu wanachama; tuna ushirika, mmoja na mwingine, kwa watu wote, madhehebu yote. Kila mtu anakaribishwa na tuwe na ushirika katika Neno la Mungu, ambapo kila mmoja angejisikia kukaribishwa kadri iwezekanavyo (2Wathesalonike 2:1-2) kwa msingi kwamba tunampenda Bwana Yesu. Na sisi siyo kundi la wasomi hapa. Tu watu wa kawaida ambao wanajaribu kusoma Biblia na hatuweki tafsiri kwake nje ya kile inachosema.

Kwa nini walisema kwamba watu wote lazima kuabudia Yerusalemu? Kwa maana kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu atashirikiana na mtu; na hapo ni chini ya damu ya ile sadaka. Hiyo ndiyo sababu ilipasa waje mpaka Yerusalemu. Mungu kamwe hatakutana na mtu mahali pengine popote ila chini ya damu. unapoikataa damu hapo sasa mahali pako pa kukutana na Mungu panaondolewa mbali. Mungu alifanya uamuzi wake wa kwanza pale bustani ya Edeni, kwamba mtu atamwabudu tu yeye chini ya damu iliyomwagwa na ile sadaka. Na hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu atakutana na watu; na hapo ndipo mahali pekee Mungu aliwahi kukutana na watu; na hapo ndipo mahali pekee yeye anakutana na watu leo, ni chini ya damu iliyomwagika ya ile sadaka (Waebrania 10:10-14).

Sasa, Waisraeli, walipokuja kwenye ushirika na Mungu, kulikuwa na mahali pamoja tu pa ushirika na Mungu, na hapo ilikuwa ni katika ile maskani. Katika maskani ndipo ambapo ile sadaka ilikuwa inaendelea kutoa damu wakati wote.

Mungu kamwe hakuahidi kukutana na watu mahali pengine popote ila chini ya damu iliyomwagika fikiria hilo. Nitaliacha hilo lizame kwa dakika sasa.

Angalia Mungu kwamwe hajaahidi kukutana na mtu yeyote katika msingi wa kustahili kwake katika msingi wa jinsi mtu mwanaume alivyo mzuri au mtu mwanamke alivyo mzuri kamwe hajaahidi kukutana nao pale. Hakuna ushirika na Mungu katika msingi wa kustahili kwako. Mahali pekee palipo na ushirika ni chini ya damu kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo nikupitia tu ile damu kitu badala, kisicho na hatia ili kufunika hatia, mwenye dhambi atubuye, ni damu peke yake.

Sasa, angalia kwa haraka Israeli aliendа katika jengo; walimwaga damu na katika jengo hili ilikuwa ni mahali pekee ambapo Mungu angekutana na kufanya ushirika na mwaminio. Katika lile jengo hapo ndipo ambapo ilikuwepo damu ilimwagwa. Yule mwanakondoo alikufa pale madhabahuni, kila siku. Ile damu iliendelea na Moshi mweusi ulining’inia juu ya

maskani. Na Mungu asingeweza kuona dhambi kwa hiyo watu walienda chini ya damu na wakawa na ushirika. (2 Mambo ya Nyakati 6-7).

Na leo tumejaribu madhehebu tumejaribu vyama tumejaribu elimu tumejaribu maendeleo ya sayansi na kila kitu kujaribu kuwaleta watu katika umoja wa ushirika. Na hiyo imeshindwa kila mmoja sasa, kuna mahali pamoja ambapo mtu anaweza akakutana na kuwa na ushirika na Mungu na ushirika mmoja kwa mwingine. Hapo ni chini ya msalaba ambapo kila mtu anaikubali Damu ya Yesu Kristo sijali katika hali zake zote zisizo za kwaida, bado anaweza akainuka na kumkuta mtu mwingine na kuweka mkononi wake juu yake kumwita yeye “ndugu” tunapokutana penye msalaba Yesu alipokufa.

Hatuwezi kukutana kama chama na kuzoza juu ya kanuni au vitu vingine vya kanisa lakini kama ndugu tunaweza kukutana chini ya damu ya mwokozi wetu Yesu Kristo na pale tunakuwa na vitu shirika.

Hicho ndicho ambacho kanisa linahitaji leo ni ushirika Chini ya

Damu ya Bwana Yesu Kristo; hata kifo hakiwezi kuitia giza.

Nimesimama kando ya vitanda vyao na kuwaangalia wakifa na kupeana mikono iliyo baridi. Nimewaona wakisimama pale na kufa, wakipiga kelele za sifa za Mungu, kwa sababu walikuwa na ushirika. Walijua ni wapi walipokuwa wamesimama oh, jinsi niwezavyo katika uzoefu mbalimbali wa kujua uzoefu kwa kuwaona watu jinsi wali……

Usijaribu kwenda kwa Mungu na chochote nje ya ushirika pamoja na Mungu, ila chini ya Damu hiyo, ndiyo njia pekee Mungu anajua kwamba hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu ataitambua lazima kwanza uoshwe kwa maji ya Neno (Yohana 15:3) halafu umeoshwa kupitia ile Damu na kuingia katika utukufu wa shekina kwenda ndani pale ndani ya ushirika hapo sasa unajua umesimamia wapi.

Sasa baada ya huyu Roho Mtakatifu kuwashukia wao, iliwafanya wakawa wapendanao sana mpaka kila kitu kilikuwa ni ushirika (matendo 2:42-47) Hiyo ni

kweli? Jamani, jamani, ushirika wa namna gani tunaimba ule wimbo wakati mwingine oh, ushirika mkuu, “oh furaha ya kimungu” ……

Lakini kwa uhalisi, kwa ukweli, kamwe hatujaonana mmoja kwa mwingine. Ulijua hilo? Hatujaonana mmoja kwa mwingine. Unasikia kitu fulani kinazungumza kutoka kwenye mwili hapa ambapo unaingiza chochote kiwacho ndani huko kwa hiyo tunapozungumza mmoja kwa mwingine hatuzungumzi hasa na mwili. Ni ile roho iliyo ndani, lakini mwili ni kitu kile kinachoitambulisha roho ambayo iko ndani. Na kwa hiyo, tunapozungumza mmoja kwa mwingine, tunaweza kwa haraka kuelewa moja kwa moja kama sisi ni Wakristo au la, kwa sababu kuna ushirika katika roho ambayo tunazungumzia katika hiyo unaona, inatingishika moja kwa nyingine kwamba tu wakristo au siyo kwa hiyo kamwe hatujaonana mmoja kwa mwingine.

Nje ya malango ya Yerusalemu aliinuliwa juu kati ya mbingu na nchi na akafa na akakomboa kila kitu, na katika kuvuja damu

alitakasa kanisa ambalo yeye mwenyewe angeweza kuishi ndani yake na kuwa na ushirika na kuzungumziana kile kitu kilichopotea cha ushirika kutoka Bustani ya Edeni ambapo Mungu alishuka chini kila jioni wakati wa kanisa.

**Nukuu za Kiingereza**

Njia Mungu aliyoiweka ya kukaribia kwenye ushirika, Aya 40-45, 36/ Edeni ya shetani uk.13/ Bartimayo kipofu (60-0330), aya 62/ Ushirika ni kwa ukombozi, Aya 170+203/ Mambo yale yatakavyo kuwa, Aya 92/ Muhuri wa pili uk 177/ Kusimama katika pengo, aya 9+19/ Lile shitaka uk. 16-18/ Mungu akijificha mwenyewe katika urahisi 63-0412E) Aya, 27/ Kitendawili (64-0206B) aya274/ Roho Mtakatifu ni nini aya107/Shalom (64-0112), aya 6/ Baraza (60-1125), Aya 30 / Kwa nini tumepewa Roho Mtakatifu Aya 29.

Jiwe la kiroho la kujengea na. 140 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E.Y. Kanju*

*Box 5138, Tanga*

*E-mail: chaelika@Hotmail.com*

*cellphone: 0784 704299*